JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

TAREHE 30/09/2026

TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

(Limetolewa kwa kuzingatia kanuni ya 7 (1)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, jumla ya shilingi **900,000,000/=** Kwa mgawanyo ufuatao :-

a) Kiasi cha fedha kwa mikopo ya vikundi vya wanawake ni shilingi **360,000,000/=**
b) Kiasi cha fedha kwa mikopo ya vikundi vya vijana ni shilingi **360,000,000/=**
c) Kiasi cha fedha kwa vikundi vya watu wenye ulemavu ni shilingi **180,000,000/=**

Fedha tajwa zimetengwa katika robo ya kwanza (Julai – Septemba) mwaka wa fedha 2026/2027, Hivyo, vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi ya Kata zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

I. Kikundi cha wanawake , vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri
II. Kikundi kiwe kinachojishughulisha nashughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali
III. Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia (5) na kuendelea. Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejiment ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zinafanana na sifa za vikundi vingine ,
IV. Kikundi kiwe na account ya benk iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
V. Wanakikundi ni lazima wawe ni raia wa Tanzania(Uthibitisho namba ya NIDA) wasio na ajira rasmi, wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kinapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroni wa **wezesha portal** ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa kata kwa usaidizi wa karibu.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatanisho vifuatavyo; barua ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa kijiji pamoja na Afisa Maendeleo ya

CamScanner

Jamii *kata husika, muhtasari wa wanachama* au kikundi wa kuomba mkopo, benki statement na andiko rahisi la mradi

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **15** mwezi **10** mwaka **2026**

Tangazo hili limetolewa na :-

Solomoni I. Shati
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
TARIME.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
TARIME

CamScanner